OFISI YA MKUU WA WILAYA YA UBUNGO

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM 2015 – 2020 KWA KIPINDI CHA KUANZIA JULAI, 2016 HADI JUNI 2017

IMETAYARISHWA NA:

WILAYA YA UBUNGO,
S.L.P. 55064
DARES SALAAM
SIMU: 0222-96341
FAX: 0222-926342

JANUARI, 2018

YALIYOMO

1 UTANGULIZI 1
1.1 TASWIRA YA WILAYA YA UBUNGO 1
1.2 MALENGO YA MPANGO WA UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM WA MWAKA 2015 – 2020 2
1.3 UTEKELEZAJI WA MALENGO YA ILANI YA UCHAGUZI KISEKTA ... 3
1.3.1 SEKTA YA ELIMU 3
1.3.2 SEKTA YA AFYA 3
1.3.3 SEKTA YA UJENZI 4
1.3.4 SEKTA YA MAJI 4
1.3.5 SEKTA YA UTUMISHI NA UTAWALA 4
1.3.6 SEKTA YA UTUMISHI NA UTAWALA 4
2 JEDWALI : UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM YA MWAKA 2015 KWA KIPINDI CHA JULAI 2016– JUNI 2017 5
2.1 JIMBO LA KIBAMBA 5
2.2 JIMBO LA UBUNGO 11

1 UTANGULIZI

1.1 TASWIRA YA WILAYA YA UBUNGO

Wilaya ya Ubungo ni moja kati ya Wilaya 5 ambazo zinaunda Mkoa wa Dar es Salaam, Wilaya nyingine ni Kinondoni, Ilala, Temeke, Kigamboni pamoja na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. Wilaya ya Ubungo ilianzishwa kwa Sheria ya Serikali (Mamlaka ya Mji) sura ya 288 kupitia (Government Notice No. 4) ya mwaka 2015.

1.2 MIPAKA NA ENEO

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo inapakana na Wilaya ya Kibaha kwa upande wa Kaskazini, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kwa upande wa Kusini - Mashariki, Wilaya ya Kisarawe kwa upande wa Magharibi. Halmashauri inaunganishwa na sehemu nyingine za miji na nchi kwa mtandao wa barabara. Barabara kuu ni pamoja na barabara ya Morogoro, Mandela, barabara ya Sam Nujoma. Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ina ukubwa wa kilomita za mraba **210.**

1.3 HALI YA HEWA

Hali ya hewa ya Manispaa ya Ubungo ni ya joto la wastani wa nyuzi joto 29^0C kwa mwaka. Kipindi cha joto huanzia kati ya miezi ya Oktoba hadi Machi, wakati kipindi cha baridi chenye kadirio la nyuzi joto 25^0C huanzia kati ya miezi ya Mei hadi Agosti na nyuzi joto 29 – 33^0C kwa miezi iliyosalia katika kipindi cha mwaka. Wastani wa mvua kwa mwaka ni mm 1,300 katika misimu miwili ambayo ni vuli miezi ya Oktoba – Desemba na Masika ambayo huanza miezi ya Machi – Mei.

1.4 IDADI YA WATU

Kwa mujibu wa Sensa ya Taifa ya idadi ya watu na makazi ya **mwaka 2012**, Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ilikuwa na idadi ya watu wapatao **845,368** ambapo wanaume ni **409,149** na wanawake ni **436,219**. Kutokana na ongezeko la ukuaji wa idadi ya watu ya asilimia 5.0 kwa mwaka,

Manispaa inakadiriwa kuwa na idadi ya watu wapatao **1,078,928** ifikapo mwaka **2017**, hivyo kila kilometa ya mraba kuwa na ujazo wa watu **5,138.**

1.5. UTAWALA

Kiutawala Wilaya ya Ubungo imegawanyika katika Tarafa **2** ambazo ni Magomeni na Kibamba, Kata **14** na Mitaa ni **91** ya utawala, Idadi ya **Majimbo ya Uchaguzi** ni mawili (2) ambayo ni **Kibamba** na **Ubungo**. Mkuu wa Wilaya ni Msimamizi Mkuu wa shughuli zote za Serikali katika Wilaya. Manispaa inaongozwa na **Baraza la Madiwani** lenye wajumbe **23** ambapo kuna Madiwani **19** na Wabunge **2** ambapo Mstahiki Meya ni Kiongozi Mkuu na Mkurugenzi wa Manispaa ni Mtendaji Mkuu kwa upande wa Serikali za Mitaa.

1.2 MALENGO YA MPANGO WA UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM WA MWAKA 2015 – 2020

Mpango wa Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM wa mwaka 2015 - 2020, umeandaliwa kwa kuzingatia maelekezo yaliyomo kwenye Ilani hiyo. Aidha, Mpango wa Utekelezaji umezingatia sera na miongozo mbali mbali ya kisekta pamoja na taarifa mbali mbali zinazokusanywa kutoka katika Halmashauri ya Ubungo. Halmashauri imedhamiria kuendelea na utekelezaji wa malengo yaliyopo katika Ilani hiyo kama ifuatavyo:-

a) Huduma ya UKIMWI kuboreshwa na maambukizi mapya kupunguzwa.
b) Uboreshaji, uendelezaji na utekelezaji kikamilifu mpango wa Taifa wa kupambana na Rushwa.
c) Kuongezeka na kuboreka kwa huduma za kiuchumi na miundombinu.
d) Kuimarika kwa Utawala bora na utoaji wa huduma.
e) Kuimarika kwa uwezo wa kiuchumi, kijinsia na ustawi wa jamii.
f) Kuimarika kwa usimamizi wa kujikinga na maafa na milipuko ya magonjwa.
g) Kuimarika kwa usimamizi wa Maliasili na Mazingira.

1.3 UTEKELEZAJI WA MALENGO YA ILANI YA UCHAGUZI KISEKTA

Katika kipindi cha Juni 2016 hadi Julai 2017 Manispaa ya Ubungo imetekeleza malengo ya Ilani ya Uchaguzi kwa kuzingatia mwongozo na taratibu za Serikali. Halmashauri imetumia jumla ya **shilingi 2,451,688,175.00** kutekeleza miradi mbalimbali kisekta.

1.3.1 SEKTA YA ELIMU

Manispaa ya Ubungo imetumia kiasi cha **shilingi 1,392,179,062.00** kutekeleza miradi ya maendeleo katika Sekta ya Elimu.

Ujenzi umefanyika katika vyumba **42** vya madarasa, matundu **96** ya vyoo na uzio katika shule ya msingi Ubungo Plaza. Aidha, Manispaa imekamilisha ujenzi wa vyumba **19** vya madarasa, matundu **24** ya vyoo na nyumba **02** za Walimu.

Ukarabati umefanyika katika vyumba **38** vya madarasa, kusawazisha na kutengeneza mifereji katika shule ya King'ongo na Saranga. Manispaa kwa kuzingatia umuhimu wa michezo kwa wanafunzi imetengeneza uwanja wa michezo na kuweka uzio katika shule ya msingi Ukombozi. Ununuzi wa vitendea kazi vya ofisi umefanyika. Jumla ya **madawati 14,837** yamenunuliwa na kusambazwa shuleni.

1.3.2 SEKTA YA AFYA

Maboresho ya huduma za afya katika Manispaa yamefanyika na kiasi cha **shilingi 157,599,900.00** zimetumika. Halmashauri imefanikiwa kutekeleza shughuli mbalimbali kama kupandisha hadhi zahanati **3** kuwa Vituo vya Afya (Kimara, Mbezi na Mburahati), kujenga vichomeo taka **02**, uzio katika zahanati ya Malambamawili, Mburahati na Mabibo na choo cha wagonjwa. Pia umefanyika ukarabati wa jengo la kujifungulia na mfumo wa maji taka zahanati ya Sinza. Manispaa imeendelea kuboresha mazingira ya zahanati kwa kutengeneza eneo la mapumziko kwa wagonjwa katika zahanati ya Mavurunza. Ukamilishaji wa zahanati ya Malambamawili umefanyika.

Aidha, Manispaa imefanikiwa kushika nafasi ya kwanza ki-mkoa katika masuala ya Usafi wa mazingira.

Manispaa imewatambua wazee **7,299** (Me 3,454 na Ke 3,845) katika Kata **11**, kati yao wazee **1,671** (Me 1,003 na Ke 668) wameshapigwa picha na kukabidhiwa vitambulisho vyao. Zoezi la Utambuzi linaendelea katika Kata **3** zilizobaki.

1.3.3 SEKTA YA UJENZI

Manispaa ya Ubungo katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Juni, 2017 imetumia kiasi cha **shilingi 550,566,100.00** katika kuboresha miundombinu. Shughuli zilizofanyika ni kukarabati barabara za Mitaa katika Kata zote 14, ujenzi wa daraja na vivuko 04 na matengenezo ya barabara yamefanyika.

1.3.4 SEKTA YA MAJI

Katika jitihada za kuimarisha usimamizi wa miradi ya maji, Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo imetumia kiasi cha **shilingi 141,861,500.00** kutekeleza Ilani ya Uchaguzi. Miradi ya maji iliyofanyika ni kukarabati na kuendeleza mradi wa maji Mpigi Magoe na kukamilisha ujenzi wa maji Kigogo Kibamba.

1.3.5 SEKTA YA UTUMISHI NA UTAWALA

Manispaa ya Ubungo chini ya Sekta ya Utumishi na Utawala katika kuboresha mazingira ya kufanyia kazi imetumia shilingi 56,241,500.00 kukamilisha ujenzi na kukarabati katika ofisi za Kata na Mitaa.

1.3.6 SEKTA YA UTUMISHI NA UTAWALA

Ili kuendeleza sera ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi Halmashauri imefanikiwa kujenga mabanda ya masoko kwa gharama ya shilingi 205,034,700.00.

MIGOGORO ILIYOWASILISHWA NA KUFANYIWA KAZI NA OFISI YA MKUU WA WILAYA YA UBUNGO

Migogoro **1,325** iliyowasilishwa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Ubungo ilitatuliwa na kufanyiwa kazi ikiwa ni pamoja na kupatiwa ushauri kwa migogoro iliyo na asili ya Kimahakama.
Migogoro mingi ni ile yenye asili ya ardhi, migogoro ya familia na ndoa, migogoro ya Vikundi vya kijamii Saccos na Vikoba na kudhulumiana.
Hata hivyo, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ubungo imeendelea kushughulikia matatizo na migogoro hiyo kwa kushirikiana na Wanasheria kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Manispaa ya Ubungo.

Mchanganuo wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo umeoneshwa katika jedwali hapo chini:-

2 JEDWALI : UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM YA MWAKA 2015 KWA KIPINDI CHA JULAI 2016– JUNI 2017

2.1 JIMBO LA KIBAMBA

NA	KATA	JINA LA MRADI	RUZUKU S/KUU	HALMASHAURI	WANANCHI	JUMLA YA FEDHA ILIPELEKWA	GHARAMA YA MRADI	UTEKELEZAJI
1.	MSIGANI	Kukamilisha madarasa 2 Shule ya Msingi Malamba mawili	0	30,000,000.00	0	30,000,000.00	28,271,300	Mradi umekamilika
		Ukarabati wa barabara za mitaa kata ya Msigani	0	4,000,000.00	0	4,000,000.00	4,000,000.00	Mradi umekamilika
		Kuweka umeme katika mradi wa maji Msingwa	0	1,000,000.00	0	1,000,000.00	1,000,000.00	Mradi umekamilika
		Ukarabati wa madarasa 8 SM Msigani	0	50,000,000.00	0	50,000,000.00	50,000,000.00	Ukarabati unaendelea
		Ujenzi wa chomeo la taka, choo, uzio na umaliziaji wa zahanati, uj ya Malambamawili	48,065,000.00	0	0	48,065,000.00	47,999,900	Mradi unaendelea
		JUMLAKATA YA MSIGANI	**48,065,000.00**	**85,000,000.00**	**0.00**	**133,065,000.00**	**131,271,200.00**	
2.	MBEZI	Ujenzi wa choo kimoja chenye matundu 12 Shule ya Msingi Makamba	32,000,000.00	0	0	32,000,000.00	30,700,000.00	Mradi umekamilika

NA	KATA	JINA LA MRADI	RUZUKU S/KUU	HALMASHAURI	WANANCHI	JUMLA YA FEDHA ILIPELEKWA	GHARAMA YA MRADI	UTEKELEZAJI
		Ukarabati wa barabara za mitaa kata ya Mbezi	0	4,000,000.00	0	4,000,000.00	4,000,000.00	Mradi umekamilika
		Ujenzi wa Daraja la Mbezi Msumi kwa Londa	0	100,000,000	0	100,000,000	249,626,000.00	Mradi unaendelea
		Kukarabati na kuendeleza miradi ya maji ya Mpiji Magohe w/s	0	42,000,000	0	42,000,000	42,000,000	Mradi unaendelea
		Kukamilisha madarasa 2 Shule ya Msingi Mshikamano	0	12,000,000	0	12,000,000	11,987,800.00	Mradi uumekamilika
		Ujenzi wa choo 1 shule ya msingi Makabe	32,000,000	0	0	32,000,000	31,691,813.00	Mradi unaendelea
		JUMLA KATA YA MBEZI	**64,000,000.00**	**158,000,000.00**	**0.00**	**222,000,000.00**	**370,005,613.00**	
3.	SARANGA	Kukamilisha madarasa 2 Shule ya Msingi Saranga	0	30,000,000	0	30,000,000	27,975,000	Mradi umekamilika
		Ukarabati wa barabara za mitaa Kata ya Saranga	0	4,000,000	0	4,000,000	4,000,000	Mradi umekamilika
		Kusawazisha na kutengeneza	0	5,000,000.00	0	5,000,000.00	5,000,000.00	Mradi umekamilika

NA	KATA	JINA LA MRADI	RUZUKU S/KUU	HALMASHAURI	WANANCHI	JUMLA YA FEDHA ILIPELEKWA	GHARAMA YA MRADI	UTEKELEZAJI
		mifereji katika s/m Saranga						
		Kusawazisha na kutengeneza mifereji katika s/m King'ongo	6,000,000.00	0	0	6,000,000.00	6,000,000.00	Mradi umekamilika
		Kukamilisha vyoo matundu 8 S/M Mavurunza	0	31,000,000	0	31,000,000	29,284,040	Mradi unaendelea
		Matengenezo ya kivuko cha waenda kwa miguu mtaa wa Upendo	15,000,000	20,000,000	0	35,000,000	34,521,300	Mradi unaendelea
		Ukamilishaji wa kivuko cha Stopover kwa Mushi	1,000,000.00	0	3,200,000.00	4,200,000.00	4,200,000.00	Ujenzi uko hatua ya maandalizi
		JUMLA KATA YA SARANGA	**22,000,000.00**	**90,000,000.00**	**3,200,000.00**	**115,200,000.00**	**110,980,340.00**	
4.	GOBA	Ukamilishaji wa ujenzi wa choo Goba mpakani Sekondari	15,000,000	0	0	15,000,000	14,739,498	Mradi umekamilika kwa kulingana mkataba
		Ujenzi wa choo sekondari ya Fahari	25,730,640	0	0	25,730,640	25,618,300	Mradi umekamilika
		Ukarabati wa barabara za mitaa kata ya Goba	0	4,000,000.00	0	4,000,000.00	4,000,000.00	Mradi umekamilika

NA	KATA	JINA LA MRADI	RUZUKU S/KUU	HALMASHAURI	WANANCHI	JUMLA YA FEDHA ILIPELEKWA	GHARAMA YA MRADI	UTEKELEZAJI
		Ujenzi wa choo sekondari ya Goba	0	32,000,000	0	32,000,000	32,000,000	Mradi unaendelea
		Kukamilisha nyumba moja ya mwalimu Shule ya Sekondari Goba	0	20,000,000	0	20,000,000	20,000,000	Hatua ya ukamilishaji
		Kukamilisha ujenzi wa nyumba ya walimu 2 kwa 1 Shule ya msingi Tegeta A	0	20,000,000	0	20,000,000	19,116,500	Mradi unaendelea
		Ujenzi wa kivuko(kalvati) kwa ajili ya kuvuka wanafunzi shule ya msingi Kunguru mtaa wa kunguru	7,300,000.00	0	0	7,300,000.00	7,300,000.00	Hatua ya manunuzi
		Ununuzi wa kompyuta 1 (desk top) shule ya Msingi Tegeta A	1,000,000.00	0	0	1,000,000.00	1,000,000.00	Hatua ya manunuzi
		JUMLA KATA YA GOBA	**49,030,640.00**	**76,000,000.00**	**0.00**	**125,030,640.00**	**123,774,298.00**	
5.	KWEMBE	Ukarabati wa barabara za	0	4,000,000	0	4,000,000	4,000,000	Mradi umekamilika

NA	KATA	JINA LA MRADI	RUZUKU S/KUU	HALMASHAURI	WANANCHI	JUMLA YA FEDHA ILIPELEKWA	GHARAMA YA MRADI	UTEKELEZAJI
		mitaa kata ya Kwembe						
		Kukamilisha vyumba 2 vya madarasa Shule ya Sekondari Luguruni (miradi viporo)	0	30,000,000	0	30,000,000	30,000,000	Mradi umekamilika
		Kukarabati madarasa 2 katika shule ya msingi Kwembe	16,000,000	0	0	16,000,000	15,918,294	Mradi umekamilika
		Ukarabati wa jengo la kujifungulia zahanati ya Kwembe	10,000,000	0	0	10,000,000	10,000,000	Maandalizi ya ukarabati yanaendelea
		Kuendeleza ujenzi wa ofisi ya mtaa Mloganzila	3,000,000.00	0	0	3,000,000.00	3,000,000.00	Ujenzi unaendelea
		JUMLA KATA YA KWEMBE	**29,000,000.00**	**34,000,000.00**	**0.00**	**63,000,000.00**	**62,918,294.00**	
6.	KIBAMBA	Ukarabati wa choo sekondari ya Kibwegere	6,000,000.00	0	0	6,000,000.00	6,000,000.00	Mradi umekamilika
		Ukarabati wa nyumba 1 ya mwalimu shule ya msingi Hondogo	14,000,000	0	0	14,000,000	14,000,000	Mradi haujaanza

NA	KATA	JINA LA MRADI	RUZUKU S/KUU	HALMASHAURI	WANANCHI	JUMLA YA FEDHA ILIPELEKWA	GHARAMA YA MRADI	UTEKELEZAJI
		Kukamilisha ujenzi wa madarasa 4 Shule ya Sekondari Kiluvya	0	35,000,000	0	35,000,000	34,899,600	Mradi umekamilika kulingana na mkataba
		Matengenezo ya kivuko cha waenda kwa miguu Kibamba	10,000,000	20,000,000	0	30,000,000	30,000,000	Maandalizi ya ujenzi
		Ujenzi wa mradi wa maji Kibamba – Hondogo	100,000,000	0	0	100,000,000	98,861,500	Mradi unaendelea
		Ukarabati wa barabara za mitaa kata ya Kwembe	0	4,000,000	0	4,000,000	4,000,000	Mradi umekamilika
		JUMLA KATA YA KIBAMBA	**130,000,000.00**	**59,000,000.00**	**0.00**	**189,000,000.00**	**187,761,100.00**	
	JUMLA KIBAMBA	**JIMBO LA**	**342,095,640**	**502,000,000**	**3,200,000.00**	**847,295,640**	**986,710,845.00**	

2.2 JIMBO LA UBUNGO

NA	KATA	JINA LA MRADI	WACHANGIAJI					
			RUZUKU S/KUU	HALMASHAURI	WANANCHI	JUMLA YA FEDHA ILIPELEKWA	GHARAMA YA MRADI	UTEKELEZAJI
1.	UBUNGO	Kukarabati shule ya Msingi Ubungo NHC	30,000,000.00	0	0	30,000,000.00	30,000,000.00	Mradi umekamilika
		Ujenzi uzio katika shule ya msingi Ubungo Plaza	0	30,000,000.00	0	30,000,000.00	29,284,000	Mradi umekamilika
		Ukarabati wa barabara za mitaa kata ya Ubungo	0	4,000,000.00	0	4,000,000.00	4,000,000.00	Mradi umekamilika
		Ujenzi wa choo SM Ubungo Plaza	0	32,000,000	0	32,000,000	31,850,000	Hatua ya ukamilishaji
		Ujenzi wa vyumba 8 vya madarasa katika shule ya msingi Ubungo Plaza	136,000,000	0	0	136,000,000	135,539,200	Hatua ya ukamilishaji kwa vyumba 7 na chumba 1 kinapauliwa
		Ukarabati wa Ofisi ya Kata Ubungo	0	16,000,000	0	16,000,000	15,555,500	Mradi umekamilika kulingana na fedha iliyopelekwa
		Ujenzi wa banda la mboga mboga Soko la shekilango-Ubungo	0	50,000,000	0	50,000,000	48,795,500	Mradi umekamilika
		Kukamilisha ujenzi wa darasa 1 S/S Urafiki	0	12,000,000	0	12,000,000	11,774,800	Mradi umekamilika
		Matengenezo ya barabara ya Msewe Golani	0	35,000,000	0	35,000,000	34,800,000	Mradi umeanza ila umesimama kutokana na kusubiri kuondolewa kwa miundombinu ya DAWASCO ili uendelee na barua

NA	KATA	JINA LA MRADI	WACHANGIAJI					
			RUZUKU S/KUU	HALMASHAURI	WANANCHI	JUMLA YA FEDHA ILIPELEKWA	GHARAMA YA MRADI	UTEKELEZAJI
								waliandikiwa barua haijajibiwa
	JUMLA KATA YA UBUNGO		**166,000,000.00**	**179,000,000.00**	**0.00**	**345,000,000.00**	**341,599,000.00**	
2	MANZESE	Ukarabati wa vyumba 5 vya madarasa shule ya msingi Kilimani	15,000,000.00	0	0	15,000,000	15,000,000	Mradi umekamilika
		Kukarabati madarasa 4 ya shule ya Msingi Uzuri	40,000,000	0	0	40,000,000	39,998,100	Mradi umekamilika
		Kukamilisha ujenzi wa Ofisi Kata ya Manzese	0	12,000,000	0	12,000,000	11,988,000	Mradi umekamilika
		Matengenezo ya barabara ya Manzese Midizini	0	10,000,000	0	10,000,000	10,000,000	Mradi umekamilika
		Ukarabati wa barabara za mitaa kata ya Manzese	0	4,000,000.00	0	4,000,000	4,000,000	Mradi umekamilika
		Ujenzi wa banda la mboga mboga Soko la Manzese Bakhresa	0	50,000,000	0	50,000,000	49,239,200	Mradi unaendelea
		Matengenezo wa uwanja wa michezo s/m Ukombozi	0	14,000,000	0	14,000,000	13,132,700	Mradi umekamilika
	JUMLA KATA YA MANZESE		**55,000,000.00**	**90,000,000.00**	**0.00**	**145,000,000.00**	**143,358,000.00**	
3.	MBURAHATI	Kukamilisha ujenzi wa choo Shule ya Sekondari Mburahati	0	1,600,000	0	1,600,000	1,600,000	Mradi umekamilika
		Ujenzi wa kichomea taka zahanati ya Mburahati	10,000,000.00	0	0	10,000,000.00	9,541,800.00	Mradi umekamilika

NA	KATA	JINA LA MRADI	WACHANGIAJI					
			RUZUKU S/KUU	HALMASHAURI	WANANCHI	JUMLA YA FEDHA ILIPELEKWA	GHARAMA YA MRADI	UTEKELEZAJI
		Ukarabati wa barabara za mitaa kata ya Mburahati	0	4,000,000.00	0	4,000,000.00	4,000,000.00	Mradi umekamilika
		Kukamilisha ujenzi wa madarasa 4 Shule ya Sekondari Mburahati	0	100,000,000	0	100,000,000	99,880,750	Mradi unaendelea
		Ujenzi wa choo cha wagonjwa zahanati ya Mburahati kata ya Mburahati	15,000,000	0	0	15,000,000	11,200,000.00	Mradi unaendelea
		Ujenzi wa choo kimoja chenye matundu 12 shule ya msingi Barafu	0	32,000,000	0	32,000,000	31,859,200	Mradi umekamilika
	JUMLA KATA YA MBURAHATI		**25,000,000.00**	**152,000,000.00**	**0.00**	**162,600,000.00**	**158,081,750.00**	
4	KIMARA	Kukamilisha madarasa 2 Shule ya Msingi Kilungule	0	15,000,000.00	0	15,000,000.00	12,474,480	Mradi umekamilika
		Ukarabati wa barabara za mitaa kata ya Kimara	0	4,000,000.00	0	4,000,000.00	4,000,000.00	Mradi umekamilika
		Ujenzi wa madarasa 8 katika shule ya sekondari mpya ya Kimara	100,000,000	0	0	100,000,000	200,000,000	Mradi unaendelea
		Ukarabati wa barabara ya Kimara Baruti – Uwanjani	0	31,200,000	0	31,200,000	31,200,000	Mradi unaendelea
		Ujenzi wa kivuko cha waenda kwa miguu Mtaa wa Baruti	3,000,000	0	0	3,000,000	3,000,000	
		Kutengeneza eneo la	6,000,000	0	0	6,000,000	6,000,000	Ujenzi upo hatua

NA	KATA	JINA LA MRADI	WACHANGIAJI					
			RUZUKU S/KUU	HALMASHAURI	WANANCHI	JUMLA YA FEDHA ILIPELEKWA	GHARAMA YA MRADI	UTEKELEZAJI
		mapumziko kwa wagonjwa Zahanati ya Mavurunza						ya kujenga kuta za msingi
	JUMLA KATA YA KIMARA		**109,000,000.00**	**50,200,000.00**	**0.00**	**159,200,000.00**	**256,674,480.00**	
5	MAKUBURI	Kuweka mfumo wa umeme Ofisi ya Kata Makuburi (ukarabati wa ofisi)	0	700,000	0	700,000	700,000	Mradi umekamilika
		Kukarabati madarasa 6 katika shule ya Msingi Makuburi	40,000,000.00	0	0	40,000,000.00	40,000,000.00	Mradi umekamilika
		Ukarabati wa barabara za mitaa kata ya Makuburi	0	4,000,000.00	0	4,000,000.00	4,000,000.00	Mradi umekamilika
		Ujenzi wa choo 1 shule ya msingi Makuburi	32,000,000	0	0	32,000,000	31,900,200	Hatua ya ukamilishaji
		Ukarabati wa vyumba 2 vya madarasa shule ya msingi Kibangu	15,000,000	0	0	15,000,000	14,985,100	Mradi umesimama anatafutwa mkandarasi mwingine
		Ukarabati wa madarasa matano (5) na ofisi moja (1) ya walimu katika shule ya Msingi Mabibo	17,977,000.00	0	0	17,977,000.00	17,977,000.00	Mradi umekamilika
		Matengenezo ya Barabara ya Makoka pattaya	0	25,357,000	0	25,357,000	24,900,000	Mradi umekamilika
	JUMLA KATA YA MAKUBURI		**104,977,000.00**	**30,057,000.00**	**0.00**	**135,034,000.00**	**134,462,300.00**	
6	MABIBO	Ukarabati wa barabara	0	4,000,000	0	4,000,000	4,000,000	Mradi umekamilika

NA	KATA	JINA LA MRADI	WACHANGIAJI					
			RUZUKU S/KUU	HALMASHAURI	WANANCHI	JUMLA YA FEDHA ILIPELEKWA	GHARAMA YA MRADI	UTEKELEZAJI
		za mitaa kata ya mabibo						
		Ujenzi wa uzio zahanati ya Mabibo	0	15,000,000	0	15,000,000	14,800,000	Mradi unaendelea
		Ukarabati wa ofisi ya kata ya Mabibo	0	10,000,000	0	10,000,000	9,998,000	Mradi umekamilika
		Ujenzi wa madarasa 6 SM Kawawa	0	102,000,000	0	102,000,000	102,000,000	Ujenzi upo hatua
		Ujenzi wa kivuko cha waenda kwa miguu mtaa wa Mabibo eneo la Kisimani	7,023,000	0	0	7,023,000	7,023,000	Wananchi wanachangishana waanze ujenzi ili fedha ya mfuko wa jimbo ikamilishe
	JUMLA KATA YA MABIBO		**7,023,000.00**	**131,000,000.00**	**0.00**	**138,023,000.00**	**137,821,000.00**	
7	SINZA	Ukarabati mfumo wa maji taka katika hospitali ya Sinza	0	55,000,000.00	0	55,000,000.00	55,000,000.00	Mradi umekamilika
		Ukarabati wa barabara za mitaa kata ya Sinza	0	4,000,000.00	0	4,000,000.00	4,000,000.00	Mradi umekamilika
		Ujenzi wa soko la mboga Sinza – Makaburini	0	50,000,000	0	50,000,000	100,000,000	Mradi unaendelea
	JUMLA KATA YA SINZA		**0.00**	**109,000,000.00**	**0.00**	**109,000,000.00**	**159,000,000.00**	
8..	MAKURUMLA	Kutengeneza kivuko cha Kilimahewa	0	18,000,000.00	0	18,000,000.00	17,995,800	Mradi umekamilika
		Ukarabati wa barabara za mitaa kata ya Makurumla	0	4,000,000.00	0	4,000,000.00	4,000,000.00	Mradi umekamilika
		Ujenzi wa mfereji wa maji ya mvua barabara	0	40,000,000.00	0	40,000,000.00	40,000,000.00	Mradi umekamilika

NA	KATA	JINA LA MRADI	WACHANGIAJI					
			RUZUKU S/KUU	HALMASHAURI	WANANCHI	JUMLA YA FEDHA ILIPELEKWA	GHARAMA YA MRADI	UTEKELEZAJI
		ya Watani mpaka Shule ya msingi Mianzini						
		Ukarabati wa ofisi ya kata ya Makurumla	0	15,000,000	0	15,000,000	15,000,000	Mradi umekamilika kulingana na fedha iliyopelekwa
		Ukarabati wa vyumba 8 vya madarasa shule ya msingi DR. Omary	0	50,000,000	0	50,000,000	49,985,000	Mradi unaendelea
		Ukarabati wa soko la Kapera	7,000,000	0	0	7,000,000	7,000,000	Fedha haitoshi imeombwa nyingine ili mradi uanze
JUMLA KATA YA MAKURUMLA			**7,000,000.00**	**127,000,000.00**	**0.00**	**134,000,000.00**	**133,980,800.00**	
JUMLA JIMBO LA UBUNGO			**474,000,000**	**868,257,000**	**0**	**1,327,857,000**	**1,464,977,330**	
JUMLA KUU JIMBO LA UBUNGO NA KIBAMBA			**816,095,640.00**	**1,370,257,000.00**	**3,200,000.00**	**2,175,152,640.00**	**2,451,688,175.00**	